

Jibu: Turejee,

Wimbo 2:9 “Mpendwa wangu ni kama paa, au ayala. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, Achungulia dirishani, atazama kimiani”.

“Kimiame” ni dirisha kubwa lililo katika **“ghorofa”**..

Madirisha makubwa yaliyo katika maghorofa tofauti na yale yaliyo katika nyumba za chini ndiyo yaliyoitwa **“kimiame”**.

Mfano wa dirisha la Kimiame ni lile ambalo mfalme Ahazia aliloanguka na kuugua..

2Wafalme 1:2 “Na Ahazia AKAANGUKA KATIKA DIRISHA la chumba chake orofani, katika Samaria, akaugua; akatuma wajumbe, akawaambia, Enendeni mkaulize kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni, kwamba nitapona ugonjwa huu”.

Na lile ambalo Yezebeli alianguka, baada ya kuangushwa na wale matowashi..

2Wafalme 9:30 “Hata Yehu alipofika Yezreeli, Yezebeli akapata habari; akatia uwanja machoni mwake, akapamba kichwa chake, akachungulia dirishani.

31 Hata Yehu alipoingia lango la mji, alisema, Je! Ni amani, Ewe Zimri, mwenye kumwua bwana wako? 32 AKAINUA USO WAKE KULIELEKEA DIRISHA, akasema, Aliye upande wangu ni nani? Matowashi wawili watatu wakachungulia.

33 Akasema, Mtupeni chini. Basi wakamtupa chini; na damu yake ikamwagika nyingine juu ya ukuta, na nyingine juu ya farasi, naye akamkanyaga-kanyaga”.

Tazama pia shubaka hapa >>>[Shubaka ni nini kibiblia? \(Mithali 7:6\)](#)

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx1>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

TOA HUDUMA ILIYO BORA.

INGIENI KWA KUPITIA MLANGO ULIO MWEMBAMBA.

KUTII NI BORA KULIKO DHABIHU.

VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 11 (Mithali, Wimbo ulio bora,

Mhubiri)

MUNGU HAJARIBIWI NA MAOVU BALI MEMA.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp

[Print this post](#)